TANGAZO LA SERIKALI NA. 174 la Tarehe 14/6/2013

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA. 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Vifungu 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO (ADA NA USHURU WA HUDUMA YA ARDHI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA ZA MWAKA 2013

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo (Ada na Ushuru wa Huduma za Ardhi) za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Jina la sheria na tarehe ya kuanza kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa Mahali pa kutumika

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itakapoelezwa vinginevyo:- Tafsiri Wajibu wa

"ada na ushuru" maana yake ni malipo yatakayotozwa na Halmashauri kwa huduma, na bidhaa zitolewazo na Halmashauri;

"biashara" maana yake ni matumizi yoyote ya kiwanja au nyumba yanayompatia au yanayopaswa kumpatia mmiliki kipato;

"eneo la jengo" maana yake ni eneo la sakafu ikijumuisha pamoja na ghorofa zote za nyumba nzima;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa;

"huduma za ardhi" maana yake ni ushauri na maelekezo ya kitaalam, upimaji kiwanja, uwekaji wa vigingi (Beacon), na kibali cha ujenzi;

"kibali" maana yake ni hati ya maandishi itolewayo na Halmashauri kumruhusu Mmiliki wa kiwanja au ardhi kuendeleza Ardhi hiyo;

"kiwanja" maana yake ni ardhi iliyopimwa iliyojengwa au inayokusudiwa kujengwa nyumba au jengo lolote;

"maombi" maana yake ni maombi ya kiwanja au shamba yanayopokelewa na Halmashauri kwa njia ya kujaza fomu maalum itolewayo na Halmashauri au maombi ya mashamba yaliyopitishwa na Halmashauri za vijiji;

"ramani" maana yake ni mchoro wa kitaalam wa jengo, viwanja, vya burudani na vinavyofanana na hivyo ulioandaliwa na mwenye kiwanja au ardhi anayopasa kuwasilisha Halmashauri kwa ajili ya kupata kibali cha kujenga;

"shamba" maana yake ni ardhi inayotumika au inayokusudiwa kutumika kwa kilimo cha mazao au ufugaji.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

4.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu kulipa Ada na Ushuru kwa Huduma au bidhaa za ardhi atakazopewa na Halmashauri.

(2) Halmashauri itatoza ada na ushuru wa huduma na bidhaa za ardhi zilizotajwa na Sheria Ndogo hizi isipokuwa huduma za ushauri na Maelekezo ya kitaalamu kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kulipa Kodi ya Kiwanja

5.-(1) Ni wajibu wa kila Mmiliki kiwanja katika Halmashauri kulipa kodi ya kiwanja hicho kila mwaka kwa viwango vitakavyotajwa na Halmashauri.

Kibali cha ujenzi

6. Mtu yeyote anayetaka kujenga au kufanya maendelezo katika kiwanja atapaswa kuomba kibali cha ujenzi kutoka Halmashauri kabla ya kuanza shughuli za ujenzi.

Makosa na Adhabu

7.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:-

(a) atajenga bila kuwa na kibali;

(b) atashindwa kulipa ada ya kiwanja;

(c) atabadilisha matumizi ya jengo au kiwanja bila kuwa na kibali;

(2) akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) na kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au faini na kifungo kwa pamoja.

JEDWALI

*(Chini ya Kifungu cha 5)*

ADA YA USHURU WA ARDHI

(i) Maombi ya kiwanja ........................................ Sh. 80,000/=
(ii) Maombi ya kupimiwa shamba au kiwanja ...... Sh. 80,000/=
(iii) Kibali cha kujenga ........................................ Sh. 20,000/=
(iv) Gharama za kupima ardhi ambayo itakuwa kwa mujibu wa kanuni zilizoainishwa katika kanuni za upimaji ardhi.
(v) Ukaguzi wa ramani ya jengo gharama zake itakuwa ni kama ifuatavyo:-

| *Matumizi ya kiwanja* | *Ada kwa mita ya mraba* |
|---|---|
| (a) Matumizi ya makazi | Tsh. 20,000/= |
| (b) Matumizi ya biashara na makazi | Tsh. 40,000/= |
| (c) Matumizi ya biashara | Tsh. 60,000/= |
| (d) Matumizi ya kiwanda | Tsh. 100,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 174 (linaendelea)*

Wilaya ya kondoa uliofanyika tarehe 27 Januari, 2012 muhtasari Na. 13/2011/2012 mbele ya:

NICHOLAS N.J KOMBE,
*Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri*

L.S.

HAMIS A. MWENDA,
*Mwenyekiti wa Halmashauri*

NAKUBALI,

Dodoma,
17 Aprili, 2013

MIZENGO PETER PINDA (MB),
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 175 la tarehe 14/6/2013

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA. 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7 (l),(b) na (e))*

SHERIA NDOGO ZA USHURU WA (MAGULIO, MASOKO NA MINADA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA ZA MWAKA, 2013

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Ushuru wa (Magulio, Masoko na Minada za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa za mwaka 2012 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la serikali. Jina la Sheria na tarehe ya kuanza kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa. Eneo la kutumika

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo; Tafsiri

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa Biashara, Afisa Mtendaji wa Kijiji au mtu yeyote aliyepewa dhamana na Halmashauri kusimamia shughuli zozote zinazoendeshwa katika gulio na mnada;

" chombo cha usafiri" maana yake ni gari la abiria, gari la mizigo na Pikipiki;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya, kamati ya maendeleo ya kata au serikali ya kijiji;

"magulio, masoko na minada" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na kumilikiwa na Halmashauri ya Wilaya au Serikali ya kijiji kwa ajili ya wafanyabiashara kununua au kuuza mazao ya chakula na biashara na hata bidhaa za viwandani;

" wakala" maana yake ni mtu yeyote, kampuni, shirika aliyeteuliwa na kupewa madaraka ya kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

*Tangazo la Serikali Na. 175 (linaendelea)*

Kutenga maeneo ya Magulio, masoko na minada

4. Halmashauri itatenga maeneo kwa ajili ya magulio, masoko na minada kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kulipa ushuru

5. (1) Mtu yeyote atakayekuwa anafanya biashara kwenye gulio, soko au mnada atawajibika kulipa ushuru kwa kiwango kilichoonyeshwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Mmiliki yeyote wa chombo cha usafiri atakayeingiza chombo hicho katika eneo ambalo gulio, soko au mnada unafanyika atawajibika kulipa ushuru wa chombo hicho kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

Uteuzi wa wakala

6. Halmashauri itateua wakala katika kila magulio, masoko na minada ambaye:-

(a) atakusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri;

(b) atatoa maelekezo na maagizo juu ya usafi, hifadhi ya mazingira na namna ya kuendesha shughuli za gulio,mnada na soko kulingana na maagizo ya Halmashauri kwa wakati mbalimbali;

(c) ataendesha na kudhibiti gulio,soko na mnada kulingana na Sheria Ndogo hizi pamoja na maagizo atakayopewa na Halmashauri kwa wakati mbalimbali.

Jukumu la Afisa Muidhiniwa

7. Ni jukumu la Afisa Muidhiniwa kuhakikisha kuwa usalama unadumishwa kwenye eneo la gulio, soko na mnada kwa kuweka utaratibu mzuri wa ulinzi wa mgambo.

8. Afisa Muidhiniwa kwa wakati unaofaa ataingia kwenye maeneo ya gulio, soko na mnada kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha Sheria Ndogo hizi zinafuatwa.

Makosa na adhabu

9 (1).Mtu yeyote atakua ametenda kosa endapo:-

(a)atakataa kulipa ushuru;

(b) atamshawishi mtu mwingine kukataa kulipa ushuru;

(c) atamzuia Afisa Muidhiniwa au Wakala kutekeleza wajibu wake.

(2) Akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja, yaani faini na kifungo.

10. Kila gulio, soko na mnada utaanza shughuli zake kuanzia saa 1.00 asubuhi hadi saa 12.00 jioni. Muda wa kufungua na kufunga magulio, masoko na minada

11. Sheria Ndogo za masoko ya Mifugo (minada) za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa 1996 sasa zimefutwa. Kufutwa kwa Tangazo la Serikali Na. 42 la tarehe 14/02/1997

JEDWALI

VIWANGO VYA ADA YA KUUZA MIFUGO

| *Aina ya Mifugo* | *Kiwango cha Ada ya Kibali* |
| --- | --- |
| Ng'ombe | Shilingi 1,000/= kwa kila ng' ombe aliyeuzwa . |
| Nguruwe | Shilingi 1,000/= kwa kila Nguruwe aliyeuzwa. |
| Punda | Shilingi 1,000/=kwa kila punda aliyeuzwa. |
| Mbuzi | Shilingi 500/= kwa kila mbuzi aliyeuzwa. |
| Kondoo | Shilingi 500/= kwa kila kondoo aliyeuzwa. |
| Aina nyingine ya mifugo ambayo haikutajwa | Shilingi 500/= kwa kila mfugo aliyeuzwa. |

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ilibandikwa katika

Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 27 mwezi Januari mwaka 2012 muhtasari Na. 13/2011/2012 mbele ya:

NICHOLAS N.J KOMBE,
*Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri*

L.S.

HAMISI A. MWENDA,
*Mwenyekiti wa Halmashauri*

NAKUBALI,

Dodoma,
17 Aprili, 2013

MIZENGO PETER PINDA,
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 176 la tarehe 14/06/2013

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7 (1), (2) na 16 (1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA, 2013

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, 2012 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa kama itakapoelezwa vinginevyo-

"Afisa muidhiniwa" ina maana ya Afisa yeyote wa umma au mtu mwingine aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa;

"hesabu" ina maana ya jumla ya mauzo au manunuzi ikiwa ni pamoja na kodi na ada, katika mwaka wa mapato;

"hesabu za mwisho" ina maana ya hesabu za mwisho;

zinazowasilishwa na Taasisi yoyote ya kibiashara baada ya kipindi cha hesabu kwa mujibu wa kifungu cha 9 ya Sheria Ndogo hizi pamoja na nyaraka au maelezo yatakayotakiwa kutolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"jumuisho" ina maana ya taarifa, nyaraka au hesabu au maelezo yoyote yahusuyo kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, zilizosambazwa, zilizotolewa na, au kuuzwa kibiashara na ikiwa ni pamoja na jumuisho la awali au la mwisho;

"kipindi cha hesabu" ina maana ya muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara zake;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mkusanya ushuru" maana yake ni mtumishi au wakala aliyeteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"mwaka wa Mapato" maana yake ni kipindi cha miezi kumi na mbili ya kalenda ya mwaka;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ,Sura ya 290;

"taasisi ya kibiashara" ina maana ya taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni au Sheria ya Majina ya kibiashara inayojihusisha na shughuli za kiuchumi za uzalishaji wa bidhaa au mazao ya kilimo, usambazaji wa bidhaa au utoaji wa huduma na, au biashara ikiwemo uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

Utozaji wa ushuru

4. Halmashauri itatoza na kukusanya ushuru wa huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kutoka kwa kila taasisi ya kibiashara katika kila mwaka wa mapato ambayo ni sawa na asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya hesabu ya shughuli zote zikiwemo za uzalishaji wa bidhaa au huduma kutoka nje ya nchi na ndani ya nchi zinazofanyika katika eneo la Halmashauri ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mlaji.

Uwasilishaji wa taarifa kuhusu shughuli za kibiashara

5. Mkurugenzi kwa taarifa ya maandishi, anaweza kumtaka mlipa ushuru au mkusanya ushuru yeyote kuwasilisha hesabu zenye taarifa kamili za shughuli za kibiashara zikionesha kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, kutolewa, kuingizwa, kusambazwa au kuuzwa kibiashara na taarifa ya fedha katika kipindi maalum kisichozidi siku thelathini tangu tarehe ya taarifa hiyo.

Uwasilishaji wa taarifa

6. Mkurugenzi anaweza kwa taarifa ya maandishi kumtaka mtu yeyote mwenye taarifa au maelezo kuhusu taasisi yoyote ya kibiashara inayopaswa kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kuwasilisha kwake taarifa au maelezo hayo katika kipindi kisichopungua siku thelathini tangu tarehe ya agizo hilo.

Uwezo wa kuingia kwenye jengo

7. Mkurugenzi anaweza kumwagiza kwa maandishi Afisa Muidhiniwa kuingia kwenye jengo au eneo la Taasisi ya kibiashara au la mlipa au mkusanya ushuru yeyote kwa nia ya kufanya uchunguzi na tathmini ya

kumbukumbu za biashara, vitabu vya hesabu, na taarifa nyinginezo kama atakavyoona inafaa kufanyiwa uchunguzi kwa ajili ya kupata na kujua kiwango sahihi cha ushuru anachotakiwa kulipa mlipa ushuru au mkusanya ushuru huo.

8.-(1) Mkurugenzi anaweza, kwa taarifa ya maandishi, kumtaka mlipa ushuru au mkusanya ushuru yeyote kuwasilisha kwake kumbukumbu za biashara na vitabu vya hesabu, kwa nia ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini au kukusanya ushuru wa huduma.

(2) Kwa nia ya kupata taarifa kwa mujibu wa Kifungu cha 8(1), Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu yeyote kufika mbele yake au kwa Afisa Muidhiniwa katika muda na mahali kadri atakavyoona inafaa.

Uwasilishaji

9. Kila mlipa au Mkusanya ushuru wa huduma atatakiwa kutoa na, au kuwasilisha hesabu za awali na kulipa ushuru unaotakiwa katika muda kama ifuatavyo:-

(a) Kwa waagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi watalipa ushuru katika muda kama itakavyokuwa imeelekezwa na Kamishina wa Kodi ya forodha na kodi ya mlaji;

(b) Wazalishaji wa bidhaa za viwandani watalipa ushuru kama itakavyokuwa imeelekezwa na kamishna wa Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT isipokuwa haitakuwa zaidi ya muda wa kulipa Kodi ya mlaji au (VAT);

(c) Watu wengine watalipa katika awamu nne (4) awamu ya kwanza ikianzia katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kuanza kwa kipindi cha mahesabu.

Uteuzi wa mkusanya ushuru

10. Mkurugenzi anaweza kuteua Kamishna wa Kodi ya forodha au kodi ya mapato kutathmini na kukusanya ushuru wa huduma na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa wakati kama ilivyoelekezwa kwenye Kifungu cha 9 kwa lengo la kufanya tathmini, kukusanya na kupata ushuru pamoja na madeni yake.

11.-(1) Kiwango cha ushuru kitakuwa ni asilimia 0.3% ya hesabu ya shughuli zote baada ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mlaji.

(2) Mkusanya ushuru au mlipa ushuru yeyote akishindwa kuwasilisha ushuru wake atachukuliwa kama hajalipa ushuru na atastahili au kuwajibika kulipa ushuru huo kama vile ndiye mlipa ushuru Halmashauri, na njia zote za kukusanya madeni zitatumika dhidi yake kama vile ndiye mlipa kodi husika.

(3) Bila ya kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi Mkurugenzi anaweza kuteua wakala kukusanya kodi kwa niaba yake na wakala huyo atakuwa na jukumu la-

(a) kuwasilisha majumuisho kwa Mkurugenzi au Afisa muidhiniwa;

(b) kuwasilisha kodi aliyokusanya katika kipindi maalum.

12.-(1) Kila mlipa ushuru au mkusanya ushuru atatakiwa kuwasilisha kwa Halmashauri hesabu za mwisho katika kipindi cha miezi minne tangu kumalizika kwa kipindi cha hesabu ya kodi anayostahili katika mkupuo mmoja.

(2) Mlipa ushuru au mkusanya ushuru anapowasilisha hesabu zake, Afisa muidhiniwa anaweza:-

(a) kupokea na kukubali hesabu hizo na kutathmini kodi katika msingi huo;

(b) kufanya tathmini kuhusu kiwango cha hesabu cha mlipa ushuru huyo iwapo atakuwa na hisia za kimsingi za kuamini kuwa hesabu hizo siyo sahihi.

(3) Iwapo mlipa ushuru hajawasilisha majumuisho ya hesabu zake kwa mwaka wowote wa pato, aidha ametakiwa kufanya hivyo na Mkurugenzi au Afisa muidhiniwa anafikiri kwamba mlipa ushuru huyo ana wajibu wa kulipa ushuru kwa mwaka huo, anaweza kwa kadri atakavyoona, kuamua kiwango cha hesabu za mlipa ushuru huyo, isipokuwa tathmini hiyo haitaathiri wajibu wowote wa mlipa ushuru anayostahili kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kwa kushindwa kwake kuwasilisha hesabu hizo.

(4) Ushuru uliotathminiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, utalipwa katika siku thelathini tangu tarehe ya kufanya tathmini.

13.-(1) Mtu yeyote anayetakiwa kulipa ushuru akishindwa kuwasilisha hesabu zake kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi katika kipindi kilichoongezwa atatozwa riba ya asilimia 1.5 kwa mwezi.

(2) Iwapo mtu yeyote atasema uongo auataficha baadhi ya hesabu zake kwa nia ya kupunguza kiwango cha ushuru anachotakiwa kulipa, na inapobainika kuwa ufichaji au upunguzaji huo aliufanya kwa makusudi, mtu huyo atatozwa ushuru pamoja na nyongeza ya ushuru ya asilimia hamsini (50%) ya tofauti kati ya ushuru anayotakiwa kulipa na hesabu alizowasilisha pamoja na kiwango cha ushuru halisi.

Jumla ya riba kutozwa kwenye ushuru isiyolipwa

14.-(1) Ushuru ambao haijalipwa kwa wakati kama ilivyoelezwa kwenye Sheria Ndogo hizi, itatozwa riba ya jumla ya asilimia 15% kwa mwezi na itatakiwa kulipwa pamoja na ushuru anayodaiwa.

(2) Riba itozwayo katika Sheria Ndogo hizi itachukuliwa kama ushuru unayòstahili kulipwa na njia zote za kukusanya ushuru na madeni zitatumika kukusanya riba hiyo kama ushuru unaolipwa na mlipa ushuru huyo.

Kushindwa kutimiza maagizo

15. Mtu yeyote ambaye bila ya sababu za msingi atakuwa ametenda kosa kama;
  (a) atasindwa kuwasilisha hesabu sahihi na za kweli;
  (b) atashindwa kuwasilisha Nyaraka, maelezo au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Halmashauri katika muda uliowekwa;
  (c) atashindwa kutunza kumbukumbu, kitabu au hesabu;
  (d) atashindwa kuonyesha kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya uchunguzi;

Makosa

16.-(1) Mtu yeyote bila ya sababu za msingi atakua ametenda kosa kama;
  (a) akifanya hesabu za uongo kwa kupunguza au kutoa hesabu zisizokuwa sahihi;
  (b) akitoa taarifa isiyokuwa sahihi kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri jukumu lake au la mtu mwingine la kulipa kodi;

(c) akiandaa au kutengeneza au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongo vya mahesabu au kumbukumbu,

(d) atamzuia au atajaribu kumzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi,

Adhabu

17.-(1) Mtu yeyote atakayevunja masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa ushuru anaodaiwa na faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au atatumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Pamoja na adhabu atakayopewa mkosaji katika Sheria Ndogo ya 17(1), mkosaji atawajibika kuilipa Halmashauri gharama iliyoingia kutokana na kuvunja masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Kufifilisha kosa

18. Endapo mtu ametenda kosa na kukiri kwa maandishi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi anaweza kushughulikia kosa hilo na kuagiza kuwa mtu huyo alipe deni analodaiwa pamoja na adhabu ya kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ilibandikwa kwenye sheria ndogo hizi kwa kuzingatia azimio la mkutano wa Halmashauri ulioitishwa na kufanyika tarehe 27 Januari, 2012 muhtasari Na. 13/2011/2012 mbele ya-

NICHOLAS N. J. KOMBE,
*Kaimu Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa*

L.S.

HAMIS A. MWENDA,
*Mwenyekiti wa Halmashauri*
*Wilaya ya Kondoa*

NAKUBALI

Dodoma,
17 Aprili, 2013

MIZENGO P. PINDA,
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 177 la tarehe 14/06/2013

SHERIA NDOGO ZA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290, 2012)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(g) (r) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA, 2013

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Jina na mwanzo wa kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa. Eneo la matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itakapoelezwa vinginevyo: Tafsiri

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri au wakala ambaye atateuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Asasi" maana yake ni vyama vya hiari, shule za umma na binafsi, magereza na taasisi za dini;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa;

"Leseni" maana yake ni leseni inayotolewa na Halmashauri;

"Mazao" maana yake ni mazao ya chakula, mazao ya biashara, mazao ya misitu na maliasili ambayo kwa kawaida kupatikana katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mnunuzi" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au taasisi yoyote inayojishughulisha na ununuzi wa mazao katika eneo la Halmashauri;

"Muuzaji" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au taasisi yoyote inayojishughulisha na uuzaji wa mazao katika eneo la Halmashauri.

Ushuru wa mazao

4.-(1) Halmashauri itaanzisha na kutoza ushuru wa mazao kutoka kwa kila mnunuzi wa mazao kwenye eneo la Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa kwenye majedwali katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Kila mnunuzi wa mazao atalazimika kulipa ushuru kabla ya kusafirisha mazao hayo.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mnunuzi aliyelipa Ushuru kuhakikisha anapewa stakabadhi ya malipo.

(4) Kila mnunuzi atatakiwa kuionyesha stakabadhi kwa Afisa Muidhiniwa endapo atakapotakiwa kufanya hivyo.

(5) Itakuwa ni marufuku kwa mnunuzi yeyote kupokea au kusafirisha mazao ambayo hayajalipiwa Ushuru kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

Kibali cha kununua mazao ya kilimo

5.-(1) Ni marufuku kwa mnunuzi, mtu yeyote, shirika, chombo kisicho cha umma kununua mazao ya kilimo ndani ya eneo la Halmashauri bila kupata kibali cha kununua mazao hayo.

(2) Kibali cha kununua mazao ya kilimo kitatolewa makao makuu ya Halmashauri au katika ofisi za Vijiji na Kata au kadri itakavyoamriwa na Halmashauri baada ya Mnunuzi huyo kulipa shilingi elfu ishirini (Ts. 20,000/=)

Kibali cha kujisajili kufanya biashara ya mazao ya misitu

6.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa mnunuzi, mtu yeyote, shirika, chombo kisicho cha umma kufanya biashara ya mazao ya misitu ndani ya eneo la Halmashauri bila kupata kibali cha kujisajili kufanya biashara hiyo.

(2) Kibali cha kununua mazao ya misitu kitatolewa na Afisa Misitu wa Halmashauri baada ya mtumiaji huyo kulipa ushuru kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Leseni za ushuru wa mazao

7. Halmashauri itatoa leseni za kuendesha shughuli za mazao ya misitu kwa kutoza ushuru wa leseni hizo kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

8.-(1) Halmashauri inaweza kumpunguzia sehemu ya ushuru au kumsamehe kabisa mtu yeyote, Taasisi, Chama cha Ushirika kulipa ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi. Msamaha

(2) Kibali hicho kitatolewa na Mkurugenzi baada ya kuidhinishwa na kamati ya fedha, Uongozi na Mipango ya Halmashauri.

9. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kukata, mti au miti kwa sababu yoyote ile isipokuwa kwa kibali maalum kitakachotolewa na Halmashauri. Marufuku kukata miti bila kibali

10. Itakuwa ni jukumu la Serikali ya Kijiji kuhakikisha kwamba:- Jukumu la serikali ya kijiji

(a) inapanda na kulinda miti kwa kuzingatia maelekezo yatayotolewa na wataalam;
(b) inasimamia utunzaji wa miti na misitu iliyomo katika maeneo yao;
(c) inatunga Sheria Ndogo zitakazozuia ukataji wa miti, ulimaji, ulishaji mifugo katika vyanzo vya maji, misitu ya asili au ya kupanda au misitu ya hifadhi na uchomaji hovyo wa moto katika maeneo yao;
(d) inatoa taarifa ya utekelezaji wa Sheria Ndogo za kijiji katika Mkutano Mkuu wa Kijiji;
(e) inatenga maeneo maalum kwa ajili ya upandaji wa miti ya aina mbalimbali ili kutunza mazingira;
(f) inasimamia kampeni za kitaifa, kimkoa na kiwilaya za kupanda miti;
(g) inatengeneza mpango mzuri wa matumizi bora ya Ardhi kwa kuzingatia shughuli za kijamii na kiuchumi zinazoendeshwa na wanakijiji wake.

11. Itakuwa ni jukumu la kila Asasi na Taasisi katika Halmashauri kuhakikisha kwamba: Jukumu la asasi

(a) inapanda miti kuzunguka maeneo yao;
(b) inashiriki katika shughuli za kupanda miti na kusaidia shughuli za uzimaji moto pale janga hilo linapotokea.

Kamati za mazingira

12.-(1) Kila Serikali ya Kijiji itatakiwa kuunda Kamati ya Kuhifadhi Mazingira.

(2) Kamati ya Kuhifadhi Mazingira itakuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji shughuli zote zinazohusiana na kuhifadhi mazingira, kulinda vyanzo vya maji na kingo za mito, ikiwa ni pamoja na kusimamia upandaji wa miti, kuzuia ukataji wa miti kiholela, kuzuia uchomaji moto ovyo na shughuli nyingine zozote zenye adhari kwa mazingira.

(3) Kamati ya Kuhifadhi Mazingira kwa kushirikiana na Afisa Mtendaji wa Kata na Afisa Mtendaji wa Kijiji itahamasisha wananchi na kutoa elimu ya Mazingira.

Uwezo wa Halmashauri

13. Halmashauri itakuwa na uwezo wa:

(a) kuziagiza Serikali za Vijiji kutenga na kutangaza eneo fulani kuwa eneo la hifadhi;

(b) kuongeza orodha ya maeneo ya hifadhi kwa madhumuni ya kutekeleza Sheria Ndogo hizi;

(c) kumuagiza mtu yeyote ambaye amevamia eneo la hifadhi kuondoka katika eneo hilo;

(d) kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kuanzisha mashamba ya miti.

Mamlaka ya Afisa muidhiniwa

14.-(1) Afisa muidhiniwa atakuwa na mamlaka chini ya Sheria Ndogo hizi kusimamisha gari lolote atakapohisi kuwa gari hilo limebeba mazao ili kuhakikisha kuwa mhusika wa gari hilo ana kibali cha mazao hayo na kwamba amelipa ushuru wa mazao hayo.

(2) Afisa muidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuzuia na kulipeleka gari au chombo chochote kilichobeba mazao kituo cha polisi litakalokuwa limebeba mazao bila kuwa na kibali na iwapo Ushuru wa Mazao hayo haujalipwa na mmiliki wa gari au chombo hicho amekataa kulipa ushuru wa mazao hayo.

(3) Afisa muidhiniwa atamtaka mmiliki wa mazao hayo kulipa Ushuru unaodaiwa na faini husika ndani ya muda wa siku 7 na iwapo mmiliki wa gari hilo hatatekeleza matakwa ya Afisa Muidhiniwa ndani ya siku 7

Afisa muidhiniwa atamfikisha mmiliki wa mazao hayo mahakamani kuomba kibali cha kuuza mazao hayo kwa mnada wa hadhara.

Marufuku

15. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote:
   (a) kubadili au kungo'oa alama za mipaka ya misitu au vyanzo vya maji;
   (b) kulima au kufanya shughuli zozote katika kingo za mito na sehemu muhimu;
   (c) kuanzisha makazi katika eneo la msitu wa hifadhi au lenye miti mingi ambalo halijafanywa kuwa msitu wa jamii pasipo kibali;
   (d) kuchunga ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda, farasi, na wanyama wengine wa aina hiyo katika kingo za mito na maeneo ya hifadhi.

Kosa na adhabu kununua mazao bila kibali

16. Mnunuzi au mtu yeyote atakayenunua mazao bila kuwa na kibali atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa sheria ndogo hizi na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini(50,000)au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja.

Kosa na adhabu ya kufanya biashara ya mazao ya misitu bila kibali cha kujisajili

17. Mnunuzi au mtu yeyote atakayefanya biashara ya mazao ya misitu bila kibali cha kujisajili atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja.

Makosa kwa ujumla na adhabu

18.-(1) Mnunuzi au mtu yeyote atakayekataa au kushindwa kulipa ushuru wa mazao atakuwa ametenda kosa kwa mujibu cha Sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa ushuru anaodaiwa na atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja.

(2) Mnunuzi au mtu yeyote atakayemshawishi mtu mwingine, Shirika, Chama cha Ushirika, Taasisi ya Serikali au Binafsi, kukataa au kukwepa kulipa ushuru, atamzuia au atajaribu kumzuia, Afisa Muidhiniwa kutekeleza wajibu wake na atakayeharibu au kuingia sehemu za misitu

ya asili bila kibali atakuwa ametenda kosa kwa mujibu cha Sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini(50,000) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja.

Kufutwa kwa Tangazo la Serikali Na. 46 la 14/2/1995

19. Sheria Ndogo za Ushuru wa Mazao za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa za mwaka 1995 sasa zimefutwa.

JEDWALI LA I

USHURU WA MAZAO YA MISITU NA VIBALI

| *Na.* | *Mazao* | *kiasi cha ushuru* | |
|---|---|---|---|
| (a) | Mkaa.................................... | Tsh. 1,000/= | kwa gunia |
| (b) | Asali.................................... | Tsh. 100/= | kwa lita moja |
| (c) | Nta........................................ | Tsh. 100/= | kwa kilogramu moja |
| (d) | Kibali cha kujisajili kufanya biashara ya mazao ya misitu.. | Tsh. 2,500/= | |
| (e) | Ushuru wa nguzo(mirunda).... | Tsh. 200/= | kwa kila mmoja |
| (f) | Mbao.................................. | Tsh. 500/= | kwa mbao moja |
| (h) | Ushuru wa gogo/slipa moja ............................ | Tsh. 200/= | kwa gogo/slipa |

JEDWALI LA II

USHURU WA MAZAO YA KILIMO

| *Na.* | *Mazao ya Kilimo* | *Kipimo kwa KGS* | *Kiwango cha Ushuru* |
|---|---|---|---|
| 1. | Alizeti | Gunia la Kg 100 | Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko |
| 2. | Karanga | Gunia la Kg 100 | Asilimia 5 ya bei ya mauzo soko |
| 3. | Mahindi | Gunia la Kg 100 | Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko |
| 4. | Mtama | Gunia la Kg 100 | Asilimia 5 ya bei ya mauzo soko |

| *Na.* | *Mazao ya Kilimo* | *Kipimo kwa KGS* | *Kiwango cha Ushuru* |
|---|---|---|---|
| 5. | Maharage | Gunia la Kg 100 | Asilmia 5 ya bei ya mauzo ya soko |
| 6. | Kunde | Gunia la Kg 100 | Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko |
| 7 | Ulezi | Gunia la Kg 100 | Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko |
| 8 | Vitunguu | Gunia la Kg 100 | Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko |
| 9 | Nyonyo | Gunia la Kg 100 | Asilimia 5 ya bei mauzo ya soko |
| 10 | Choroko | Gunia la Kg 100 | Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko |

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ilibandikwa kwenye sheria ndogo hizi kwa kuzingatia azimio la mkutano wa Halmashauri ulioitishwa na kufanyika tarehe 27 Januari, 2012 muhtasari Na. 13/2012/ 2012 mbele ya-

NICHOLAS N. J. KOMBE,
*Kaimu Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa*

L.S.

HAMISI A MWENDA,
*Mwenyekiti wa Halmashauri*
*Wilaya ya Kondoa*

NAKUBALI

Dodoma,
17 Aprili, 2013

MIZENGO P. PINDA,
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 178 la tarehe 14/06/2013

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7 (1) na 16 (1)*

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA, 2013

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, 2013 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Jina na tarehe ya kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Kondoa. Eneo la matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo- Tafsiri

"ada na ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa ajili ya huduma, vibali na leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa;

"matangazo na mabango" maana yake ni maandishi yeyote yaliyoandikwa au kubandikwa kwenye vibao, ukuta wa jengo au chombo chochote kwa ajili ya kutangaza biashara;

"madini ya ujenzi" maana yake ni mawe, kokoto, mchanga, moramu na udongo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kondoa pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"plinth area" maana yake ni eneo la jengo lililotumika kujenga;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290;

"taka" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi mazingira ya Mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya

hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka;

"taka ngumu" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi mazingira Na 20 ya Mwaka 2004 ni taka ambazo haziko katika umajimáji kutoka majumbani. Katika majengo ya biashara, viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi plastic au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu (scraps);

"taka za viwandani" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, maana yake ni Uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyotiwa dawa, au mawasiliano, pamoja na taka nyinginezo ngumu kama zilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004 sehemu ya IX;

"uchafu hatari" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia, kwa binadamu au mazingira;

"wakala" maana yake ni mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au Taasisi iliyoteuliwa na Halmashauri kutoa huduma zinazohusiana na Sheria Ndogo hizi.

Ada na ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza na kukusanya Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya huduma mbalimbali, vibali na leseni zitolewazo kama ilivyoainishwa kwenye majwedali mbalimbali katika Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru utozwao chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma au leseni au kibali husika.

(3) Ada na Ushuru zitozwazo zitalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake ambaye atatoa stakabadhi ya Halmashauri kama kielelezo cha kukubali malipo hayo.

Ada ya unyonyaji maji taka

5. Halmashauri itatoza ada ya unyonyaji maji taka kulingana na viwango vilivyoanishwa katika jedwali la sheria ndogo hizi.

6. Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa ada au ushuru kulipa ada na ushuru kama zilivyoelekezwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi. Wajibu wa kulipa ada na ushuru

7.-(1) Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni atatakiwa kuwa na regista ya kuandika majina ya wageni watakaolala katika wageni katika nyumba hiyo. Regista katika nyumba za kulala wageni

(2) Regista hizo zitatolewa na Halmashauri kwa kulipia ada ambayo itapangwa na Halmashauri.

(3) Regista hiyo itapaswa kuwa na majina kamili ya mgeni huyo,sahihi mahali anapotoka, mahali anapokwenda na kiasi cha fedha alicholipa kwa siku kwa ajili ya kulala katika nyumba hiyo ya wageni.

(4) Itakuwa ni kosa kwa mmiliki wa nyumba ya wageni kulaza wageni katika nyumba hiyo bila kuandika majina ya wageni waliolala katika nyumba hiyo katika regista.

8. Afisa muidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia katika nyumba ya kulala wageni muda wowote kwa ajili ya kufanya ukaguzi, kumtaka mtu yeyote anayetakiwa kulipa ada, ushuru au kodi kufanya malipo hayo kwa mujibu wa sheria ndogo hizi. Mamlaka ya Afisa Muidhiniwa

9.-(1) Endapo mtu yeyote anayetakiwa kulipa ada au ushuru atashindwa kulipa ndani ya muda unaotakiwa kulipa, Halmashauri inaweza kukusanya ada hizo kwa njia ya Mahakama. Ukusanyaji wa madeni

(2) Bila ya kuathiri masharti yaliyowekwa na kifungu cha (1) hapo juu, Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ada kwa njia ya kukamata na kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la Ada au Ushuru.

(3) Baada ya siku thelathini (30) kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada. Uwezo wa kuuza mali zilizokamatwa na kushikiliwa utakuwa halali iwapo Mkurugenzi, kwa maandishi atatoa taarifa ya kusudio la kuuza mali hizo endapo mwenye mali atashindwa kulipa deni analodaiwa pamoja na adhabu ndani ya kipindi cha siku kumi na nne (14).

*Tangazo la Serikali Na. 178 (linaendelea)*

Uwezo wa Afisa Muidhiniwa

10. Afisa Muidhiniwa anaweza kuingia katika jengo lolote kwa nia ya kukusanya ada au ushuru.

Makosa na adhabu

11. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote:
   (a) atakataa au atakwepa kulipa Ada na Ushuru anaopaswa kulipa;
   (b) atamshawishi mtu yeyote au kundi la watu wasilipe Ada na Ushuru huo kwa namna yoyote ile bila sababu ya msingi;
   (c) akiwa ni wakala akishindwa kuwasilisha kiasi cha Ada au Ushuru alichokusanya na katika wakati muafaka.

Makosa na adhabu

12. Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia, atatakiwa kulipa ushuru unaodaiwa na atatozwa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000.00) au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili (12) jela au vyote kwa pamoja, faini na kifungo.

Kufutwa kwa Tangazo la Serikali Na. 47 la tarehe 14/ 02/1997

13. Sheria ndogo za Ushuru na Ada za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa za mwaka 1996 sasa zimefutwa.

Kufutwa kwa tangazo la serikali Na.179 la tarehe 19/ 06/2009

14. Sheria ndogo za (Ushuru wa vibao vya Matangazo ya biashara za Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa za mwaka 2009 sasa zimefutwa.

GHARAMA ZA UNYONYAJI MAJI MACHAFU

| | |
|---|---|
| (1) *Unyonyaji maji taka*: | |
| (a) Viwandani, Taasisi na Mashirika | Sh. 50,000.00 kwa safari |
| (b) Maeneo ya biashara | Sh. 50,000.00 kwa safari |
| (c) Maeneo ya makazi | Sh. 30,000.00 kwa safari |

USHURU WA MATANGAZO YA BIASHARA

| | |
|---|---|
| 1 Matangazo ya maonyesho | |
| (a) Ikiwa ya ndani ya nchi | Sh. 5000.00kwa siku |
| (b) Ikiwa ya kutoka nje ya Wilaya | Sh. 30,000.00 kwa siku |
| 2 Matangazo ya biashara | |
| (a) Matangazo kwa kutumia vipaza sauti | Sh. 5000.00 kwa siku. |
| (b) Matangazo kwa kutumia gari na maonyesho ya video | Sh. 20,000.00 kwa siku. |

3 Matangazo ya wasanii.
(a) Ikiwa kutoka ndani ya nchi — Sh. 20,000 kwa siku
(b) kutoka nje ya nchi — Sh. 30,000 kwa siku.

4 Matangazo ya maandishi kwa kila mita

| Aina ya tangazo | Kiasi cha ushuru |
|---|---|
| (a) Yasiyowaka ya kudumu | Tsh. 80,000.00 kwa mita za eneo kwa mwaka. |
| (b) Yanayowaka ya kudumu | Sh. 50,000 kwa mita za eneo |

ADA YA KUCHIMBA BARABARA

| | | |
|---|---|---|
| (1) | Kukata barabara ya lami | ............Sh. 50,000 kwa mita |
| (2) | Kukata barabara ya kifusi | ............Sh. 15,000 kwa mita |
| (3) | Kukata barabara ya udongo | ............Sh. 2,000 kwa mita |
| (4) | Kukata pembezoni mwa barabara kusikosakafiwa mjini | ............Sh. 2,000 kwa mita |

USHURU WA MADINI YA UJENZI

| | | |
|---|---|---|
| 1) | Tani 1 – 3½ | Sh. 2,000.00 kwa safari |
| 2) | Tani 4 – 7 | Sh. 3,000.00 kwa safari |
| 3) | Tani 8 na kuendelea | Sh. 5,000.00 kwa safari |

USHURU WA MACHINJIO

| *Aina ya myama* | *Ushuru* |
|---|---|
| 1. Ng'ombe | Sh. 3000.00 kwa kila ng'ombe atakayechinjwa |
| 2. Mbuzi | Sh. 1000.00 kwa mbuzi atakayechinjwa |
| 3. Kondoo | Sh. 1000.00 kwa kondoo atakayechinjwa. |
| 4. Nguruwe | Sh. 2000.00 kwa kila nguruwe atakayechinjwa |

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ilibandikwa kwenye sheria ndogo hizi kwa kuzingatia azimio la mkutano wa Halmashauri ulioitishwa na kufanyika tarehe 27 Januari, 2012 muhtasari Na. 13/ 2011/2012 mbele ya-

NICHOLAS N. J. KOMBE,
*Kaimu Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa*

HAMIS A. MWENDA,
*Mwenyekiti wa Halmashauri*
*Wilaya ya Kondoa*

NAKUBALI

Dodoma,
17 Aprili, 2013

MIZENGO P. PINDA,
*Waziri Mkuu*